JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MIFUMO YA TIKETI MTANDAO ILIYOIDHINISHWA KUTOA HUDUMA KWA MABASI YAENDAYO MIKOANI NA NCHI JIRANI

***Dar es Salaam, 30 Januari, 2026***

### 1. Utangulizi

Kanuni za Tiketi Mtandao za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024, zilizotangazwa na Serikali (**Tangazo la Serikali Na. 23 la tarehe 12 Januari, 2024)**, zinaweka sharti kwamba **mifumo yote ya Tiketi Mtandao inapaswa kujaribiwa, kuidhinishwa, na mmiliki wake kupata kibali cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA)** ili itumike rasmi kutoa huduma kwa vyombo vya usafiri wa umma.

Aidha, viongozi mbalimbali wa Serikali wakiongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamekuwa wakisisitiza juu ya azma ya Serikali kuhakikisha malipo ya miamala yafanyika kupitia mifumo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kuuaga mwaka 2025 na kuukaribisha mwaka mpya 2026 alieleza kuwa ***"Tunaanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya mwaka 2050 ambapo Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa muda wa Kati wa miaka mitatu toka mwaka 2026 hadi 2028 kwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato, kufanya malipo na kuongeza umakini katika kukusanya fedha na raslimali za umma"***

### 2. Vigezo vya Kuidhinisha Mfumo wa Tiketi Mtandao

Kwa mujibu wa **Kanuni ya 5** ya Kanuni hizo, Mfumo wa Tiketi Mtandao unaostahili kupewa kibali unapaswa kutimiza vigezo vifuatavyo:-

a) uwe unamilikiwa na taasisi ya Serikali, chama cha ushirika au kampuni iliyosajiliwa Tanzania;

b) uwe umeunganishwa na mfumo wa usimamizi wa malipo ya mapato wa kielektroniki;

c) uwe una uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya Mamlaka, Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao, na mfumo wowote kama inavyohitajika;

d) uwe umeidhinishwa na mamlaka zinazohusika;

e) uwe wa kitanzania;

f) uwe na mmiliki mwenye wafanyakazi wenye taaluma husika; na
g) uwe na ulinzi dhidi ya vamizi za kimtandao.

Utekelezaji wa vigezo hivi vya kisheria unalenga kuwawezesha wasafirishaji **kupata mapato ya mauzo ya tiketi kwa ufanisi bila kupitia watu wa kati**, kuwasaidia abiria **kununua tiketi kwa uwazi, urahisi, bila ulanguzi**, na kuiwezesha Serikali **kusimamia sekta ya usafiri kwa ufanisi zaidi**, huku kila mdau akitimiza wajibu wake ipasavyo.

**3. Hatua Zilizochukuliwa na Mamlaka Kuidhinisha Mifumo ya Tiketi Mtandao**

Mamlaka imeendelea kutoa elimu na kushirikiana kwa karibu na wadau wa usafirishaji ikijumuisha wajengaji wa mifumo ya Tiketi Mtandao (E-Tickets Vendors) ili kuhakikisha utekelezaji kamili wa Kanuni hizi, kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za usafiri zilizo **bora, salama, zenye kuaminika na kuongeza ufanisi** kwa wasafirishaji, watumia huduma (abiria) na Serikali. Utekelezaji huu unafanyika kwa ushirikiano wa **wamiliki wa mifumo ya tiketi mtandao na wataalamu wa mifumo wa Serikali, hususani, Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA)**.

Tangu kuanza kwa utekelezaji wa Kanuni za tiketi mtandao mwezi Oktoba 2024, Mamlaka imekaa vikao zaidi ya 7 na watoa huduma wa mifumo ya tiketi mtandao vikilenga kuwapa elimu na kuwakumbusha Matakwa ya usajili yanayotakiwa kutekelezwa ili kuruhusiwa kutoa huduma. Katika vikao hivyo, pamoja na mambo mengine, Mamlaka na watoa huduma walikubaliana kuwa, hadi kufikia tarehe **31 Juni 2025** watoa huduma wote wawe wamekamilisha matakwa yote yanayotakiwa kutekelezwa ili kuruhusiwa kutoa huduma. Hata hivyo, hadi kufikia **30 Disemba 2025** ni watoa huduma 5 tu kati ya 15 ndio waliokuwa wamekamilisha matakwa hayo. Tarehe **30 Disemba 2025** Mamlaka ilitoa taarifa ya muda wa mwisho wa kukamilisha matakwa kuwa tarehe **14 Januari 2026**.

**4. Kampuni na Mifumo ya Tiketi Mtandao Iliyoidhinishwa na LATRA**

Hadi leo, **tarehe 30 Januari, 2026**, jumla ya **mifumo 10 ya tiketi mtandao** imekidhi vigezo vya kisheria na kuidhinishwa kuendelea kutoa huduma.

Kampuni na Mifumo yao ya Tiketi Mtandao iliyoidhinishwa na LATRA ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1 lifuatalo:

**Jedwali Na. 1: Kampuni na Mifumo ya Tiketi Mtandao Iliyoidhinishwa**

| SN | JINA LA MTOA HUDUMA | JINA LA MFUMO |
|---|---|---|
| 1 | AB Courier Express Limited | AB Connect |
| 2 | Busbora Company Limited | Busbora |
| 3 | Hashtech Tanzania Limited | MySafari tiketi |
| 4 | Iyishe Company Limited | Iyishe Company Limited |
| 5 | Logix Company Limited | Msafiri |
| 6 | Mkombozi Infotech Company | Baspoa |
| 7 | Otapp Agency Company Limited | Otapp |
| 8 | Sepatech Company Limited | Afritech |
| 9 | Voltic Tanzania Limited | Voltic Tanzania Limited |
| 10 | Web Corporation Limited | Web e-ticketing |

**Chanzo:** LATRA 2026

## 5. Kampuni na Mifumo ya Tiketi Mtandao Iliyozuiliwa kutoa huduma

Mifumo mingine yote ya tiketi mtandao, tofauti na ile iliyotajwa hapo juu, imeshindwa kukidhi matakwa ya kisheria licha ya kupewa muda wa kutosha kurekebisha mapungufu yaliyoainishwa. Kwa mujibu wa sheria, mifumo hiyo haitambuliki na Mamlaka na hairuhusiwi kuendelea kutoa huduma. Mifumo hiyo ni pamoja na ifuatayo:

**Jedwali Na. 2: Makampuni na Mifumo ya Tiketi Mtandao Iliyozuiliwa kutoa huduma**

| SN | JINA LA MTOA HUDUMA | JINA LA MFUMO |
|---|---|---|
| 1. | Exabytes Africa Ltd | Exabytes Tiketi |
| 2. | Global Light & Company Limited | Tiketi Rafiki |
| 3. | Duarani Innovat limited | Safari Yetu |
| 4. | Itule Company Limited | Safiri Tiketi |

**Chanzo:** LATRA 2026

Mtoa huduma wa tano kati ya wale 15, alikuwa ni msafirishaji ambaye kwa sasa hatoi tena huduma za tiketi mtandao. Hata hivyo, tunatoa wito kwa kampuni ambazo mifumo yao ya tiketi mtandao haijakidhi vigezo kuendelea kukamilisha taratibu za kisheria, na itakapokamilisha na kuidhinishwa, itaruhusiwa rasmi kutoa huduma.

**6. Maelekezo kwa Watoa Huduma kwa Mabasi Yaendayo Mikoani na Nchi Jirani**

Kuanzia tarehe ya taarifa hii, wamiliki wa mabasi wanaelekezwa kutumia mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa pekee. Wasafirishaji ambao kwa sasa wameunganisha mabasi yao kwenye mifumo isiyoidhinishwa wanapewa muda wa siku 14 hadi tarehe 15 Februari, 2026 kuhamia kwenye mifumo iliyoidhinishwa. Baada ya tarehe hiyo, hawataruhusiwa kutoa huduma kwa kutumia mifumo isiyoidhinishwa. Aidha, kuanzia tarehe hiyo, utoaji na uhuishaji wa leseni za usafirishaji wa abiria utazingatia matumizi ya mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa.

Aidha, wasafirishaji wanakumbushwa kutumia wahudumu (makondakta) waliosajiliwa LATRA na wahudumu wahakikishe kila abiria anatiketi ya mtandao.

**7. Maelekezo kwa Abiria**

Kuhakikisha unanunua Tiketi Mtandao mwenyewe kupitia mfumo tumizi wa safari tiketi unaopatikana Play Store, AppStore au kwa anwani ya tiketi.latra.go.tz. Pia abiria watumie mfumo tumizi wa LATRA App kuhakiki tiketi na nauli halali. Pia abiria akiwa na malalamiko anakumbushwa kuwasilisha malalamiko kwa Mtoa Huduma kwanza, kisha kama hajaridhika na suluhisho la msafirishaji alete malalamiko LATRA. Namba za kituo cha LATRA cha huduma kwa wateji ni 0800110019/20.

**8. Hitimisho**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini inatoa shukrani za dhati kwa wasafirishaji, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) pamoja na Wamiliki wa Mabasi mkoa wa Arusha na Kilimanjaro (AKIBOA), wamiliki wa mifumo ya tiketi mtandao, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na wadau wengine wote kwa ushirikiano wao katika kutekeleza Kanuni za Tiketi Mtandao na kuboresha huduma za usafiri nchini.

***Pamoja kwa Usafiri Bora***

Digitally Signed By Salum PAZZY
Fri Jan 30 17:07:10 EAT 2026

Salum PAZZY

**MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO**